Nasaha za ´Allaamah Ahmad an-Najmiy juu ya kitabu

Rifqan Ahl-as-Sunnah bi Ahl-is-Sunnah

Mwandishi:

´Allaamah Ahmad bin Yahyaa an-Najmiy

Tarjama:

Abu Bakr Khatwiyb al-Atrush

Kwenda kwa muheshimiwa Shaykh na ´Allaamah ´Abdul-Muhsin bin Hamad al-´Abbaad al-Badr:

as-Salaam ´alaykum wa Rahmatullaah wa Barakaatuh

Amma ba´d:

Ndugu yangu mpendwa! Nilipokea simu kutoka kwako usiku wa alhamisi 10-05-1424 ukilaumu kwamba umesikia sauti yangu nikimjibu muulizaji ya kwamba hakuna ambaye anaeneza kitabu chako kinachoitwa "Rifqan Ahl-as-Sunnah bi Ahl-is-Sunnah" isipokuwa mtu mzushi. Mimi nakwambia yafuatayo:

Allaah anajua vyema kuwa sikukufanyia Tabdiy´ na wala sikukudia kukufanyia Tabdiy´. Mimi nakuzingatia ni katika Ahl-us-Sunnah wenye kupambana katika kueneza [Sunnah]. Lakini ninachoamini ni kwamba kuandika kwako kitabu hiki umeteleza katika Sunnah ambayo bado mpaka sasa unaieneza na kuwafunza watu tangu hapo kale, ingawa naamini kabisa kuwa hukukusudia hivyo. Lakini madai yako ilikuwa ni kutaka kuleta suluhu baina ya pande mbili:

Upande wa kwanza ni ule wenye hamasa ambao kwa hamasa zao wanatoka katika njia ya kati na kati.

Upande wa pili ni ule ulio kati na kati.

Lakini uhakika wa mambo ni kwamba ulikosea kutunga kitabu hiki ambacho udhahiri wake ni kuwavunja moyo Salafiyyuun juu ya kuwazungumzia na kuwakosoa Ahl-ul-Bid´ah.

Pili: Kinadhihirisha kuwatia makosani kwa yale yanayopitika kwao kuwazungumzia Ahl-ul-Bid´ah, kuwalaumu kwa hilo na kuwaaibisha.

Tatu: Badala ya kwamba kuwazungumzia Ahl-ul-Bid´ah iwe ni aina moja wapo ya ´ibaadah inayomkurubisha mtu kwa Allaah, umefanya kuwa ni tendo kubwa la jinai. Imaam Ahmad bin Hanbal aliulizwa:

"Kuna mtu mmoja anaswali, anafunga na anasoma Qur-aan. Kuna mwingine ambaye anawazungumzia Ahl-ul-Bid´ah; [yupi bora kati ya hao wawili?]. Akajibu: "Yule

anayeswali, anafunga na kusoma Qur-aan manufaa yanamrudilia yeye mwenyewe. Ama kuhusu ambaye anawazungumzia Ahl-ul-Bid´ah manufaa yanaenea kwa watu kwa kule kuwatahadharisha kwake na Ahl-ul-Bid´ah."

Nne: Ahl-ul-Bid´ah wametumia fursa msimamo wako huu na wakakufanya kuwa ni mwenye kuwatetea na kuwagombania. Wamekieneza kitabu chako mamia ya kopi, bali maelfu ya kopi - hizo ndio khabari zilizotufikia. Tazama ni kina nani waliofaidika na umesimama katika safu ya kina nani juu ya kitabu hiki.

Tano: Hakika unatakiwa kutambua kuwa umewasaidia Salafiyyuun na kuwatetea kama ambavyo vilevile umewasaidia wazushi na kuwatetea. Mambo ni hivyo sawa uwe umejua hilo au hukujua.

Ni wepi waliokifurahikia kitabu chako na ni kina nani kilichowasikitisha. Hakuna shaka ya kwamba kimewafurahisha Hizbiyyuun na kuwasikitisha Salafiyyuun. Salafiyyuun wanakuombea Allaah akurudishe katika haki na wanakuombea akujaalie miongoni mwa watetezi na wenye kuilinda Sunnah kama alivyokujaalia kuwa mmoja katika wale wenye kuieneza.

Sita: Miaka thelathini iliyopita nilisoma kitabu chako "Takhriyj twuruq Hadiyth". Hapo ndipo nilipozidi kukuheshimu na kukupenda. Na bado mpaka sasa nasikia kuwa una darasa kuhusu Hadiyth. Nimesikia pia baadhi ya mizunguko ya kielimu kwenye Redio masiku machache yaliyopita. Vilevile nimesikia namna unavyowachambua wapokezi wa milolongo ya wapokezi. Nilitamani na mimi Allaah aniwafikishe kuwahifadhi wapokezi wa Hadiyth kama wewe.

Saba: Si vinginevyo bali ni kwamba kitabu hiki kimekuangusha pale uliposema kuwa kumzungumzia mzushi ni usengenyaji. Ukweli wa mambo ni kwamba unajua kuwa kusengenya ni kumsema mtu vibaya pasi na kuwa na malengo ya kutetea dini. Ama mtu akikusudia kuitetea dini haiwi kusengenya. Wewe [pindi unapofundisha Hadiyth] ni lazima utaje kuwa fulani ni Murjiy au kwamba anatuhumiwa Irjaa´, mwengine alikuwa anaonelea maoni ya Khawaarij, mwingine Qadariy au kwamba alikuwa anatuhumiwa Qadar. Ukisema kuwa huku ni kusengenya - na ni kweli kusengenya ni haramu - basi na sisi tutakwambia kuwa ni haramu kwako kuwasengenya watu na kula nyama zao. Na ikiwa utasema kuwa kusengenya inajuzu ikiwa lengo ni kutetea dini, basi na sisi hali kadhalika tutakwambia kuwa inajuzu kusema kuwa fulani ni mzushi ikiwa tunakusudia kumtahadharisha ili Bid´ah zake zisisambae.

Nakubaliana na wewe ya kwamba haijuzu kumzungumzia mtu ambaye haijulikani hali yake. Lakini pale atapofanya Bid´ah na akanasihiwa, lakini pamoja na hivyo akakataa kukubali, hapo atasuswa na kuachwa.

Nane: Dalili ya kujuzu kusengenya ikiwa mtu amekusudia kutahadharisha ni nyingi. Zipo katika Qur-aan na Sunnah na wakazithibitisha Salaf katika Maswahabah, Taabi´uun na maimamu wa Athar waliokuja baada yao. Miongoni mwa dalili za Qur-aan ni maneno ya Allaah (´Azza wa Jall):

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ جَاهِدِ الْكُفَّارَ وَالْمُنَافِقِينَ وَاغْلُظْ عَلَيْهِمْ ۚ وَمَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ ۖ وَبِئْسَ الْمَصِيرُ

"Ee Nabii! Pambana na makafiri na wanafiki na kuwa mgumu kwao. Makazi yao ni Motoni - na ubaya ulioje mahali pa kuishia!"[1]

Hii inawahusu wanafiki wenye unafiki wa kiitikadi na wenye unafiki wa kimatendo. Ndani yake wanaingia wazushi.

Miongoni mwa dalili za Sunnah, al-Bukhaariy amepokea kupitia kwa ´Aaishah (Radhiya Allaahu ´anhaa) aliyasema: "Kuna mwanaume alibisha hodi kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Alipomuona akasema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam): "Mtu mbaya aliyoje wa kabila lake! Mtoto mbaya aliyoje wa kabila lake!" Alipoketi (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akamuonyesha uso wa bashasha na kumfanyia tabasamu. Mwanaume yule alipoenda, ´Aaishah akasema: "Ee Mtume wa Allaah! Ulipomuona ulisema hivi na hivi lakini hata hivyo umemuonyesha uso wa bashasha na kumfanyia tabasamu." Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akasema: "Lini uliwahi kuniona nikisema vibaya? Hakika watu waovu kabisa wataokuwa na nafasi mbaya siku ya Qiyaamah ni wale wanaotengwa na watu kwa ajili ya kuepuka shari zao."[2]

Vilevile Hadiyth ya Faatwimah bint Qays inayosema kuwa Abu ´Amr bin Hafsw alimpa talaka ya mwisho wakati alikuwa hayupo. Wakili wake akamletea shayiri lakini hakuipenda. Akasema: "Ninaapa kwa Allaah huna juu yetu haki yoyote." Faatwimah akaenda kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na kumweleza ambapo akamwambia: "Huna haki ya matumizi kwake." Akamwamrisha aende kukaa eda nyumbani kwa Umm Shariyk kisha akasema: "Yule ni mwanamke ambaye watu wangu wanamwogopa. Nenda kakae eda kwa Ibn Umm Maktuum, ni mwanaume kipofu na unaweza kuyapunguza mavazi yako. Pindi eda yako itapokwisha nijuze." Faatwimah anasema: "Pindi eda yangu

[1] 09:73

[2] al-Bukhaariy (6032)

ilipokwisha nikamwambia kuwa Mu´aawiyah bin Abiy Sufyaan na Abu Jahm wote wawili wamenichumbia." Ndipo Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akasema: "Kuhusu Abu Jahm haishushi bakora yake kutoka shingoni mwake. Mu´aawiyah ni masikini hana pesa. Olewa na Usaamah bin Zayd." Pamoja na hivyo mimi sikupenda. Akanambia tena: "Olewa na Usaamah bin Zayd." Nikaolewa naye na Allaah akajaalia kheri kwake."[3]

Mfano wa hilo ni Hadiyth ya ´Aaishah aliyesimulia: "Hind bint ´Utbah, mke wa Abu Sufyaan, aliingia kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallaam) na kusema: "Ee Mtume wa Allaah! Abu Sufyaan ni mwanaume bakhili hanipi matumizi ya kunitosheleza mimi na wanangu. Isipokuwa [natoshelezwa] mpaka nichukue kutoka katika mali yake pasi na yeye kujua. Je, nina dhambi kwa hilo?" Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallaam) akasema: "Chukua katika mali yake kwa wema kile kitachokutosheleza wewe na wanao."

´Abdullaah bin Mughaffal alimwona mtu anarusha jiwe ambapo akamwambia: "Usirushe jiwe, kwani Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallaam) amekataza kurusha jiwe au alikuwa akichukizwa na kurusha jiwe." Baada ya hapo akamuona anarusha jiwe ambapo akamwambia: "Nimekweleza kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallaam) amekataza au amechukizwa na kurusha jiwe halafu wewe unarusha? Sintokuzungumzisha kwa muda fulani."[4]

Kumepokelewa mfano wa hayo kutoka kwa Abiy Bakrah (Radhiya Allaahu ´anh).

Kuhusu yaliyopokelewa kutoka kwa Salaf kuna mengi. Miongoni mwa hayo ni yale yaliyosimuliwa kutoka kwa Shu´bah bin al-Hajjaaj ya kwamba amesema:

"Njoo tusengenye kwa ajili ya Allaah (´Azza wa Jall)."

Imesimuliwa pia kutoka kwa ´Aaswim bin Ahwal (Rahimahu Allaah) aliyesema:

"Qataadah alikuwa akimponda ´Amr bin ´Ubayd. Nikajishika kwenye magoti yangu na kusema: "Ee Abal-Khattwaab! Wanachuoni wanapondana namna hii?" Akasema: "Ee Ahwal! Mtu aliyezua Bid´ah ni bora kutajwa kuliko kumnyamazia."

al-Hasan bin ar-Rabiy´ amesimulia ya kwamba Ibn-ul-Mubaarak amesema:

[3] al-Nasaa´iy (3245).

[4] al-Bukhaariy (5479) na Muslim (1954).

"Mu´allaa bin Hilaal ndiye mwenyewe pamoja na kuwa inapokuja Hadiyth husema uongo." Baadhi ya Suufiyyah wakasema: "Ee Abu ´Abdir-Rahmaan! Unasengenya?" Akasema: "Nyamaza! Tusipobainisha ni vipi itajulikana haki kutokamana na batili?"

´Abdullaah bin Ahmad amesema: "Nilimuuliza baba yangu maoni yake kuhusu Ahl-ul-Hadiyth; kwa sababu wakati mwingine anakuja mwalimu pengine akawa ni Murji-ah, Shiy´ah au akawa na kitu kinachoenda kinyume na Sunnah. Ni sawa nimnyamazie au nitahadharishe naye?" Baba yangu akasema: "Ndio, tahadharisha naye ikiwa anaita na kulingania katika Bid´ah na ndio kiongozi wao."

al-Hasan al-Baswriy (Rahimahu Allaah) amesema:

"Ahl-ul-Bid´ah hawana kusengenywa."

´Affaan (Rahimahu Allaah) ameeleza: "Tulikuwa tumekaa kwa Ismaa´iyl bin ´Ulayy wamoja wakizungumza na wengine. Nikasema: "Huyu sio imara." Mwanaume mmoja akasema: "Umesengenya." Ismaa´iyl akasema: "Hakusengenya, alichofanya ni kuhukumu kuwa sio imara."

Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

"Mtu akidhihirisha maovu ni wajibu kumtahadharisha hadharani na atakuwa hakubaki na kusengenywa. Vilevile itakuwa ni wajibu kumkosoa hadharani kwa yale yanayopelekea kumtia khofu katika kumsusa na mengine."[5]

Ibn-ul-Jawziy amesema:

"Imaam Abu ´Abdillaaah Ahmad bin Hanbal kutokana na kushikamana kwake barabara na Sunnah na kutahadharisha Bid´ah alikuwa akiwazungumzia kundi katika wabora wanapofanya kitu kinachokwenda kinyume na Sunnah. Maneno yake hayo yanazingatiwa kuwa ni kutoa nasaha kwa ajili ya dini."[6]

Kwa jumla ni kwamba kuna mapokezi mengi kutoka kwa Salaf. Hayawezi kupata nafasi yote katika jibu hili fupi. Kuna mapokezi vilevile kutoka kwao ambayo yanashaji´isha kumkemea yule ambaye kunadhihiri kutoka kwake yale yanayokwenda kinyume na Shari´ah, ambaye anatoa maneno yanayoweza kufasiriwa haki na batili kwa wakati mmoja au akawa anachanganya kati ya Sunnah na Bid´a.

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

[5] Majmuu´-ul-Fataawaa (28/217).

[6] Manaaqib Imaam Ahmad bin Hanbal, uk. 185

"Mfumo wa Salaf na maimamu ni kwamba wanazingatia maana sahihi inayojulikana na Shari´ah na akili kama ambavyo vilevile wanazingatia matamshi ya Kishari´ah. Wanayaeleza kiasi na uwezo wao. Mwenye kuzungumza kwa maneno yenye maana batili yanayoenda kinyume na Qur-aan na Sunnah, anaraddiwa. Anayetamka kwa matamshi ya kizushi ambayo yanaweza kufasiriwa haki na wakati huo huo yakafasiriwa batili, atanasibishiwa Bid´ah vilevile na kuambiwa: "Amekabili Bid´ah kwa Bid´ah na kuraddi batili kwa batili."[7]

Amesema tena: "Misingi ya dini ni miwili:

1- Tusimuabudu mwengine asiyekuwa Allaah mmoja.

2- Kumuabudu kwa yale aliyoyawekea Shari´ah. Kwa msemo mwingine tusimuabudu kwa Bid´ah. Amesema (Ta´ala):

لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا

".. ili akujaribuni ni nani kati yenu anayetenda matendo mema zaidi."[8]

Fudhwayl bin ´Iyaadhw amesema kuhusu Aayah hiyo:

"Maana yake ni yenye *ikhlaasw* na yenye kusibu." Akaambiwa: "Maana yake ni nini?" Akasema: "Kitendo kikiwa kimefanywa kwa ajili ya Allaah pekee na kisiwe chenye kuafikiana na Sunnah hakikubaliwi, na kikiwa ni chenye kuafikiana na Sunnah na kisiwe kimefanywa kwa ajili ya Allaah hakikubaliwi. Mpaka kiwe na yote mawili... "

Ibn Taymiyyah akaendelea kusema:

"Ikiwa wanachuoni [watavutana] katika hali zao, maneno, mema, maovu, uongofu, upotevu, mwongozo na kupinda basi wayaridisha kwa Allaah na kwa Mtume. Wayakubali yale yenye kukubaliwa na Allaah na Mtume wake na warudishe yale yenye kurudishwa na Allaah na Mtume wake."[9]

Dini yetu imejengwa juu ya mambo matatu:

1- Kumuamini Allaah.

[7] Dar´ Ta´aarudhw-il-´Aql wan-Naql, uk. 254

[8] 67:02

[9] Majmuu´-ul-Fataawaa (27/22)

2- Kuamrisha mema.

3- Kukataza maovu.

Allaah (Ta´ala) amesema:

كُنتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ

"Mmekuwa Ummah bora kabisa ulioteuliwa kwa watu: mnaamrisha mema na mnakataza maovu na mnamwamini Allaah."[10]

Muslim amepokea katika "as-Swahiyh" yake kupitia kwa ´Ubaadah bin Waliyd bin ´Ubaadah bin as-Swaamit ambaye kapokea kutoka kwa baba yake na baba yake kapokea kutoka kwa babu yake aliyesema:

"Tulimpa *Bay´ah* Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) juu ya kusikia na kutii katika hali nyepesi na nzito, uchangamfu wetu na kuchukia kwetu, pindi kutapendelewa juu yetu, tusivutane na wenye jambo lao na tuseme haki popote tulipo - tusikhofu juu ya Allaah lawama za mwenye kulaumu."

Katika upokezi mwingine kumekuja nyongeza:

"... isipokuwa mpaka pale mtapoona kufuru ya wazi mlio na dalili kwayo kutoka kwa Allaah."

Kuanzia kwenye dalili hizi inapata kubainika kuwa Allaah (´Azza wa Jall) amewaamrisha waja wake kuamrisha mema na kukataza maovu na waseme hali popote walipo - pasi na kujali kwa ajili ya Allaah lawama za mwenye kulaumu. Hili ndilo lililonifanya kusema haki ninayoijua. Nilichokisema ni kwamba: Shaykh ´Abdul-Muhsin ni katika Ahl-us-Sunnah na hatuna lolote la kumtuhumu. Lakini hata hivyo amekosea kuandika kitabu hiki. Kwa ajili hii ndio maana Ahl-ul-Bid´ah walifurahi na wakawa wakanieneza kwa kiwango kikubwa.

Tisa: Pengine unaweza kusema kuwa hukukusudia kuwanyamazia wazushi na kwamba hujamwambia yeyote kuwanyamazia na kwamba umekusudia kukhafifisha mizozo inayoendelea baina ya Salafiyyuun. Nakujibu ifuatavyo:

Uwajibu wako na kwa mwengine ambaye anazungumzia jambo kama hili ni yeye kupambanua anapohukumu kati ya Salafiyyuun na Hizbiyyuun mpaka ibainike hukumu ya kila kundi kivyake na khaswa ukizingati ya kwamba Khawaarij wa zama hizi wamekuwa ni wenye kutumia *Taqiyyah* kwa hali ya juu.

[10] 03:110

Kumi: Umesema kuwa msimamo wa Ahl-us-Sunnah juu ya mwanachuoni pale anapokosea ni kuwa anapewa udhuru na wala hafanyiwi Tabdiy´ na wala hatengwi kwa kutumia dalili ya wanachuoni watatu waliotangulia; al-Bayhaqiy, an-Nawawiy na Ibn Hajar. Hawa ni kweli waliteleza katika kuzifasiri kimakosa baadhi ya sifa za Allaah (Ta´ala) na wana vitabu vikubwa na vyenye faida. Kwa ajili hiyo ndio maana Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wameona kuwa watu wana haja ya kufaidika na vitabu vyao katika yale yasiyokuwa na zile Bid´ah walizotumbukia ndani yake. Wanafunzi wanatakiwa kutahadharishwa kutokamana na Bid´ah zao na wakati huo huo wafaidike na vitabu vyao katika yale ambayo wamepatia. Lakini sijui kwamba Ahl-us-Sunnah waliwapa udhuru katika zile sifa za Allaah walizozifasiri kimakosa na kuyaita hayo kuwa ni "Bid´ah".

Halafu isitoshe umetoa mfano mwingine kwa Shaykh al-Albaaniy ambaye ni mmoja katika wanachuoni wa Ahl-us-Sunnah wa sasa ambaye alikuwa na maoni ya peke yake katika baadhi ya mambo ambayo yanatokamana na Ijtihaad inayoweza kusemwa kuwa ni dhaifu. Pamoja na kuwa yamejengwa juu ya dalili ambazo yeye alikinaika nazo. Huu ni mfano usiyokuwa mahala pake. Sisi tunachozungumzia ni kuwasusa Ahl-ul-Bid´ah tofauti na al-Albaaniy ambaye hayuko katika wao. Ameitumikia Sunnah na mapokezi usiku na mchana kwa kuzigawanya, kuzikosoa, kuzisahihisha na kuzidhoofisha. Ole wako kumtaja mahali kama hapa!

Vilevile umeleta maneno ya baadhi ya Salaf yaliyo kwa sura ya jumla na hukuorodhesha yaliyojaa kwenye vitabu kuhusu kuwasusa wazushi. Ni lazima iwe tayari umeshasoma vitabu hivyo au baadhi yake ikiwa ni pamoja na:

1- "al-Ibaanah al-Kubraa" na "as-Sughraa" ya Ibn Battwah.

2- "Sharh-us-Sunnah" ya al-Laalakaa´iy.

3- "as-Sunnah" ya Ibn Abiy ´Aaswim.

4- "ash-Shariy´ah" ya al-Aajurriy.

Kuna vitabu vinginevyo walivyoandika mapokezi ya Salaf kuhusu kuwakata wazushi.

Kuyanyamazia mapokezi hayo yanakufanya kuwa ni mwenye kuhojiwa mbele ya Allaah kabla ya kuhojiwa na watu.

Shaykh! Umesahau kuwa Imaam wa Ahl-us-Sunnah Ahmad bin Hanbal (Rahimahu Allaah) aliwaamrisha watu kumsusa Husayn bin ´Aliy al-Karaabiysiy, kutochukua elimu kutoka kwake na kutosoma vitabu vyake. Akatupiliwa mbali na hakuna aliyechukua elimu kutoka kwake pamoja na kuwa alikuwa na elimu kubwa.

Vilevile aliamrisha kumsusa Sahl bin ´Abdillaah at-Tusturiy ambaye alikuwa akiitwa "Sahl mfupi" na kutosoma vitabu vyake. Ahl-ul-Hadiyth wakaachana naye. Daawuud bin ´Aliy adh-Dhwaahiriy alikataa asiingie kwake.

Ahl-us-Sunnah vilevile walimkata al-Hasan bin Swaalih bin Hayy pindi walipojua Bid´ah yake.

Shaykh! Mimi sijui mapokezi haya umeyasahau au umejifanya kuyasahau?

Shaykh! Mimi nakunasihi baada ya kuinasihi nafsi yangu kufuata mapokezi ya Salaf na kupita juu ya uongofu na mfumo wao.

Shaykh! Unajua kuwa kosa analofanya mwanachuoni fulani katika hukumu za mataga ambazo inajuzu kufanya Ijtihaad ndani yake ndilo ambalo anapewa udhuru mwenye nalo na wala haitofaa kumfanyia Tabdiy´ wala kuhamwa. Kosa analofanyiwa Tabdiy´ mwenye nalo na kukatwa ni lile linalohusiana na ´Aqiydah. Hatujui kuwa Salaf kuna mtu ambaye alizua katika ´Aqiydah kisha wakampa udhuru.

Kumi na moja: Umesema kuwa Salafiyyuun wamegawanyika katika makundi mawili kwa sababu ya watu wawili. Nafikiri kuwa unamaanisha Shaykh Rabiy´ bin Haadiy al-Madkhaliy na Abul-Hassan Sulaymaan al-Maghribiy. Mimi nakwambia:

Masuala yanahusiana na haki inayotakiwa kunusuriwa na kusapotiwa na batili inayotakiwa kupondwa na kubainishwa ubatilifu wake. Tuhuma zako hizi kuwaelekezea Salafiyyuun - wanachuoni na wanafunzi - ni kuwatuhumu kuwa na ubaraka na ushabiki wenye kuchukiwa ambao Allaah amewatakasa nao pale aliposema (Jalla wa ´Alaa):

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُونُوا قَوَّامِينَ لِلَّهِ شُهَدَاءَ بِالْقِسْطِ ۖ وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَآنُ قَوْمٍ عَلَىٰ أَلَّا تَعْدِلُوا ۚ اعْدِلُوا هُوَ أَقْرَبُ لِلتَّقْوَىٰ

“Enyi mlioamini! Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Allaah mkitoa ushahidi kwa uadilifu na wala chuki ya watu isikufanyeni kutokufanya uadilifu.”[11]

al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kupitia kwa ´Ubaadah:

"... tuseme haki popote tulipo - tusikhofu juu ya Allaah lawama za mwenye kulaumu."

Haya na mfano wake ndio yaliyotufanya sisi kusema haki ingawa hayo yatapelekea baadhi ya watu kuchukia.

[11] 05:08

Shaykh! Unaona kuwa sisi tunafuata mfumo wa watu waliokuwa katika kipindi kabla ya kuja Uislamu na wapotevu ilihali Allaah amezitia nuru nyoyo zetu kwa Qur-aan na Sunnah? Maangamivu kwa mwenye kufanya hivo!

Watu wawili ambao Ahl-us-Sunnah wamegawanyika kwa sababu yao - kwa mujibu wa maneno yako - ni jambo lisilowezekana kabisa wote wawili wakawa juu ya haki halafu kila mmoja akawa kinyume na mwenzie. Hilo litalazimisha mmoja awe juu ya haki na mwingine awe juu ya batili. Batili hii iliyo na huyo mwingine ima iwe ni batili tupu au batili iliyochanganyika na haki. Inajulikana kuwa Allaah ametuamrisha kuifuata haki, kuinusuru na kuwanusuru watu wake:

اتَّبِعُوا مَا أُنزِلَ إِلَيْكُم مِّن رَّبِّكُمْ وَلَا تَتَّبِعُوا مِن دُونِهِ أَوْلِيَاءَ ۗ قَلِيلًا مَّا تَذَكَّرُونَ

“Fuateni yale mliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wenu na wala msifuate badala Yake walinzi. Ni machache mnayoyakumbuka.”[12]

وَأَنَّ هَٰذَا صِرَاطِي مُسْتَقِيمًا فَاتَّبِعُوهُ ۖ وَلَا تَتَّبِعُوا السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن سَبِيلِهِ ۚ ذَٰلِكُمْ وَصَّاكُم بِهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ

“Hakika hii ni njia Yangu iliyonyooka, basi ifuateni, na wala msifuate njia za vichochoro vikaja kukufarikisheni na njia Yake - hivyo ndivyo alivyokuusieni kwayo mpate kucha.”[13]

Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Mnusuru ndugu yako sawa akiwa ni mwenye kudhulumu au mwenye kudhulumiwa." Wakasema: "Huyu [tumeelewa kumnusuru] akiwa ni mwenye kudhulumiwa. Vipi tutamnusuru [huyo mwingine] akiwa ni mwenye kudhulumu?" Akasema: "Mzuie kutokamana na dhuluma zake."[14]

Allaah ametuamrisha kufuata Shari´ah Yake, kwa kuwa ndani yake mna haki safi kabisa isiyokuwa na utatizi. Hilo ni kwa kuwa Allaah ameisema vibaya batili na watu wake na akatukataza kuichanganya haki na batili na vilevile kuficha haki. Amesema (Ta´ala):

وَلَا تَلْبِسُوا الْحَقَّ بِالْبَاطِلِ وَتَكْتُمُوا الْحَقَّ وَأَنتُمْ تَعْلَمُونَ

[12] 07:03

[13] 06:153

[14] al-Bukhaariy (6952).

“Wala msichanganye haki kw batili na mkaficha haki na hali kuwa mnajua.”[15]

يَا أَهْلَ الْكِتَابِ لِمَ تَلْبِسُونَ الْحَقَّ بِالْبَاطِلِ وَتَكْتُمُونَ الْحَقَّ وَأَنتُمْ تَعْلَمُونَ

“Enyi Ahl-ul-Kitaab! Kwanini mnachanganya haki kwa batili na mnaficha haki na hali ya kuwa mnajua?”[16]

Atayefuatilia wanayozozana watu hao wawili itambainikia yafuatavyo:

Mosi: Shaykh Rabiy´ anajulikana vyema kulingania kwake katika Sunnah, kuijua kwake kikamilifu na kupambana kwake tangu hapo zamani kwa ajili yake.

Pili: Shaykh Rabiy´ ametunga vitabu ambavyo vingi katika hivyo amewaraddi wale wenye kwenda kinyume na Sunnah. Lengo ni kuitetea Sunnah na kupambana kwa ajili yake. Hatujui kuwa amekhalifu dalili katika suala hata limoja. al-Albaaniy (Rahimahu Allaah) amemshuhudilia hivo.

Kuhusu Abul-Hasan ni kijana aliyeghurika ambaye ameandika vitabu kadhaa ambavyo hakusibu haki tupu na kutembea pamoja na dalili. Bali ametolewa makosa. Huku ni kwa njia ya kuwatazama wote wawili kwa njia ya jumla.

Tukimtazama Abul-Hassan kwa njia ya upambanuzi basi tutaona kuwa anatilia shaka mapokezi yaliyopokelewa kupitia njia moja - خبر الآحاد- pale yatapokuwa yamesihi kwa mujibu wa kanuni za kiistilahi. Huku ni kwenda kinyume na Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah na kufuata maoni ya Mu´tazilah na wale wenye kufuata nyayo zao.

Pili: Anaonelea kufasiri maneno ya jumla ya wanachuoni kwa kutumia yaliyo wazi. Huku ni kwenda kinyume na yale waliyomo Salaf. Hakufanywi hivo isipokuwa katika maneno ya yule aliyekingwa na kukosea (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Tatu: Anawatweza na kuwadharau Ahl-us-Sunnah na kuwaadhimisha wazushi. Anasema kuhusu Ahl-us-Sunnah kwamba ni wafitinishaji, watu wadogo, wachanga na maneno mengine ya dharau. Upande mwingine anawaonelea wazushi kama mlima. Alijibu pindi alipoulizwa kuhusu al-Maghraawiy:

"Vipi nitaweza kuliondosha jibali kubwa?"

[15] 02:42

[16] 03:71

Nne: Anawapa udhuru wazushi. Mmoja wao ni Sayyid Qutwub ambaye amethibitisha mwanzoni mwa Suurah "al-Hijr" ya kwamba Ummah wa Muhammad umeritadi kutoka katika dini yote na kwamba hakuna nchi wala jamii ya Kiislamu inayotendea kazi Shari´ah ya Allaah[17]. Vilevile amethibitisha katika Suurah "Yuunus" ya kwamba misikiti ya waislamu ni hekalu za kishirikina na akaifasiri Suurah "al-Ikhlaasw" kwa Wahdat-ul-Wujuud.

Tano: Anampa udhuru Maghraawiy Takfiyriy.

Sita: Hufikia kwa wazushi ambao wanampokea sehemu zote anapofikia. Haanasiki isipokuwa kwao tu.

Saba: Aliulizwa kuhusu al-Ikhwaan al-Muslimuun kama ni katika Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ambapo akajibu: "Ndio."

Nane: Wamemshuhudilia wanaume katika wanachuoni ambao wanaaminiwa kwa elimu yao ya kwamba wamemjaribu uongo katika mambo mengi.

Hii ndio hali ya Abul-Hasan. Vipi basi utasema kuwa Ahl-us-Sunnah wamegawanyika makundi mawili kwa sababu ya watu wawili. Maneno yako uliyonizungumzisha kwenye simu yanafahamika kuwa watu hawa wote wawili ni katika Ahl-us-Sunnah. Hivi kweli ni sahihi kusema kuwa Abul-Hasan ni katika Ahl-us-Sunnah pamoja na majanga alionayo? Hapana. Ni sahihi ya kwamba wafuasi wake ni katika Ahl-us-Sunnah? Hapana. Ikiwa unaonelea kuwa Abul-Hasan na wafuasi wake ni katika Ahl-us-Sunnah, basi sisi tunasitika juu ya hilo na tunakunasihi kurejea kutoka katika maoni haya.

Umesema:

"Hii leo kumepitika fitina ya kujeruhi na kususa kutoka kwa baadhi ya Ahl-us-Sunnah ambao wameshughulika na kujeruhi na kutahadharisha, jambo ambalo limepelekea katika mfarakano na kutofautiana... Hilo linatokamana na sababu mbili:

1- Kuna Ahl-us-Sunnah hii leo ambao kazi yao kubwa ni kupeleleza na kupekua makosa. Ni mamoja iwe makosa hayo yanapitika katika vitabu au mikanda. Baada ya hapo wanamtahadharisha yule mwenye makosa hayo."[18]

Hii ni sifa nzuri na sio mbaya. Kuitetea Sunnah ilikuwa ni sifa nzuri kwa Salaf. Vijana wa ki-Salafiy wana ghera pindi wanapoona kitu kinachoenda kinyume na Sunnah kwenye

[17] (04/2122) .

[18] Uk. 44

kitabu au kwenye mkanda au wakaona kutoka kwa Ahl-us-Sunnah ambaye anatembea na Ahl-ul-Bid´ah baada ya nasaha, wanakemea hilo na kutoa nasaha au wanaomba nasaha kutoka kwa wanachuoni. Ataponasihiwa na asinasihike wanamsusa. Hii ni sifa nzuri kwao na si mbaya.

Kisha ukasema:

"Miongoni mwa makosa hayo ambayo mtu anakatwa na kutahadharishwa kwayo ni kushirikiana na baadhi ya jumuiya/taasisi kwa kutoa muhadhara au kushiriki katika daura ilihali Shaykh ´Abdul-´Aziyz bin Baaz (Rahimahu Allaah) na Shaykh Muhammad bin ´Uthaymiyn (Rahimahumaa Allaah) walikuwa wakitoa mihadhara kwenye jumuiya hizi kupitia njia ya simu na mtu anaashiriwa kidole katika jambo ambalo wanachuoni hawa wawili watukufu wamefutu kufaa kuliingia."

Jumuiya hii si nyingine bali ni Ihyaa´ at-Turaath iliyoko Kuwait inayosimamiwa na ´Abdur-Rahmaan ´Abdul-Khaaliq ambaye ana makosa na kuwafanyia mzaha Salafiyyuun.

Umesema:

"Katika nyakati mbalimbali bado waislamu mpaka hii leo wanajitokeza watu ambao wanadai kuinusuru dini na kuzungumza haki. Watu hao wanawaacha wenye kuabudu mizimu, washirikina na makafiri na kalamu yao inatumika kwa waislamu tu. Bali tumewaona baadhi yao ambao hawana kazi nyingine isipokuwa kuwashughulikia walinganizi wanaolingania katika dini ya Allaah kwa kuwatukana, kuwaaibisha mpaka kufikia kutunga vitabu vinavyobainisha mifumo yao... "

Huku ni kuwatukana Salafiyyuun, kuwakejeli na kukaripia mfumo wao pindi wanapowakemea wazushi. Walinganizi wanaolingania katika dini ya Allaah anaowakusudia si wengine isipokuwa ni al-Ikhwaan al-Muslimuun, Suruuriyyuun, Qutbiyyuun, Takfiyriyyuun na Khawaarij ambao wanafanya maandalizi kwa ajili ya kufanya uasi. Tulipokuwa tunasema mfano wa hawa walikuwa wakipinga. Ama hii leo Allaah amewafedhesha kutokana na milipuko, risasi zinazoonekana na vifaa vingine wanavyojiandaa kwayo kwa ajili ya kufanya uasi. Bali ´Abdur-Rahmaan ´Abdul-Khaaliq katika maneno yake kuna yenye kuthibitisha kuwa yeye mwenyewe ni Takfiyr. Amesema alipokuwa akimalizia maneno niliyonukuu hapo juu:

"Hii ni dhambi kubwa na ni moja katika vitenguzi vya msingi wa imani. Vilevile ndio msingi wa kupenda kwa ajili ya Allaah."

Hapa anadai kuwa kuwazungumzia wazushi ni katika mambo yanayotengua Uislamu wa mtu. Huu ni mfumo wa Takfiyriyyuun. Maneno yake hayo niliyonukuu nimeyatoa kwenye

kitabu "Qudwaat-ul-Kibaar bayn at-Ta´dhwiym wal-Inbihaar" kilichoandikwa na Muhammad Muusa ash-Shariyf, uk. 66-67. Kipande cha maneno yake haya niliyonukuu ameyaashiria kwenye makala inayozungumzia kuhusu kupenda na kuchukia kwa ajili ya Allaah aliyoandika ´Abdur-Rahmaan ´Abdul-Khaaliq.

Namalizia kwa kusema: Shaykh ´Abdul-Muhsiyn! Shaykh Ibn Baaz na Shaykh Ibn ´Uthaymiyn kutoa mihadhara kwenye jumuiya hizi kitendo hicho hakizitakasi. Huenda walifanya hivo kabla ya kujua kuwa zina makosa.

Unaonelea kuwa watu wasitiwe majaribuni na unadai kuwa ni Bid´ah. Jua - Allaah akujuze - ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alimjaribu mjakazi kwa kumuuliza: "Allaah yuko wap?" Akasema: "Juu ya mbingu." Akamuuliza tena: "Mimi ni nani?" Akasema: "Wewe ni Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ndipo akasema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam): "Mwache huru, kwani hakika ni muumini."

Baadhi ya Salaf wamesema:

"Alama ya Ahl-ul-Bid´ah ni kuwasema vibaya Ahl-ul-Athar."

Wamesema tena:

"Ukimuona mtu wa Kuufah anamtukana Sufyaann ath-Thawriy, basi utambue kuwa ni Shiy´iy. Ukimuona mtu wa Marwaz anamtukana ´Abdullaah bin al-Mubaarak, basi utambue kuwa ni Jahmiy."

Wamesema vilevile:

"Anayetuficha Bid´ah zake hatutofichikana na matangamano yake."

Bi maana atajulikana kuwa ni mzushi kwa kuangalia ni nani anayetangamana na kuungana naye. Mtu hawezi kutangamana na kuungana isipokuwa tu na wale ambao ameridhia mfumo wao.

Hii ni nasaha fupi kutoka kwa ndugu kwenda kwa ndugu yake ambayo nimependa kukuzindua katika baadhi ya mambo. Ninamuomba Allaah (Jalla Sha´nuh) azitengeneze hali za wote na atuthibitishe katika yaliyo na kheri duniani na Aakhirah. Kwani hakika Yeye ni mwenye kusikia na yukaribu.

Tunamuomba Allaah atukinge na ushabiki wenye kuchukiwa, ayafanye matendo yetu ni yenye kufanywa kwa ajili ya kukusudia Uso Wake na radhi Zake.

Swalah na salaam zimwendee Mtume wetu Muhammad, kizazi chake na Maswahabah wake.

Imeandikwa na:

Ahmad bin Yahyaa an-Najmiy